

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI



MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASWA

Telegrams "MAJI Tel No: 028-2750237/2750375

S.L.P 185, Maswa

Fax: 028-27502337, Barua pepe: mdmauwasa@maji.go.tz

MKATABA MDOGO WA AJIRA ZA MAFUNDI

KATI YA

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASWA

S.L.P 185, MASWA, SIMIYU

NA

FUNDI MJENZI BAHATI LUCAS MWAIPOPO WA S.L.P 2968, MWANZA

KWA

**KUCHIMBA MITARO KUJENGA VITUO VYA KUCHOTEA MAJI, KUJENGA
CHEMBA ZA MAJI, KULAZA MABOMBA NA KUFUKIA KWA AJIRI YA
KUSAMBAZA MTANDAO WA MAJI MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA
MAZINGIRA MASWA**

MKATABA NA. MAUWASA/2020/21/W/12

NOVEMBA 2021

MKATABA WA FUNDI MJENZI



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASWA

Telegrams "MAJI Tel No: 028-2750237/2750375

S.L.P 185, Maswa

Fax: 028-27502337, Barua pepe: mdmauwasa@maji.go.tz



BAHATI LUCAS MWAIPOPO
S.L.P 2968,
MWANZA

16/11/2021

**YAH: KUSHINDA ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA FUNDI MJENZI WA
KUCHIMBA MITARO, KUJENGA VITUO VYA KUCHOTEA MAJI, KUJENGA
CHEMBA ZA MAJI, KULAZA MABOMBA NA KUFUKIA KWA AJIRI YA
KUSAMBAZA MTANDAO WA MAJI MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA
MAZINGIRA MASWA**

Husika na mada tajwa hapo juu.

Rejea maombi yako ya Zabuni kutoa huduma ya Fundi Mjenzi wa Kuchimba Mitaro, Kujenga Vituo vya Kuchotea maji, Kujenga Chemba za Maji, Kulaza Mabomba na Kufukia kwa ajiri ya Upanuzi Mtandao wa maji Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Maswa iliyowasilishwa na kufunguliwa tarehe 10/11/2021. Nachukua fursa hii kukutaarifu kuwa bodi ya zabuni Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Maswa imekutunuku zabuni hii kwa kiasi cha fedha za kitanzania Shilingi Milioni Themanini na moja laki nne elfu tano tu. (Tsh 81,405,000.00). baada ya kukidhi vigezo

Utatekeleza mkataba huu ni ndani siku 14 baada ya kusainiwa. Hivyo kwa barua hii unatakiwa kufika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Maswa tarehe 17/11/2021 siku ya Jumanne kwa ajili ya kusaini mkataba

Nakutakia maandalizi mema ya kufanya kazi hii.

Inj. Nandi Mathias
Mkurugenzi Mtendaji
MAUWASA-WSSA

MKURUGENZI MTENDAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA
USAFI WA MAZINGIRA MJINI MASWA
P.O. Box 185, MASWA

MKATABA HUU unafanyika leo tarehe 17 mwezi 11mwaka 2021

BAINA YA

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASWA (MASWA-WSSA), MKOA WA SIMIYU S.L.P 185, SIMIYU (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri kwa upande mmoja;

NA

BAHATI LUCAS MWAIPOPO , MASWA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiriwa au Fundi") kwa upande mwingine.

KWAMBA kwa pamoja Mwajiri na Mwajiriwa watajulikana kama pande mbili za Mkataba.

AMBAPO:

- a) Mwajiri ni Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Maswa mwenye jukumu la kutekeleza ujenzi wa mradi wa kujenga jengo la ofisi katika mji wa Maswa.
- b) Mwajiriwa ni mtu binafsi anayefanya shughuli zake binafsi za ujenzi **MASWA**
- c) Mwajiri anakusudia kumwajiri Mwajiriwa kwa kipindi cha muda mfupi wa miezi sita(6);

Mwajiriwa anakubali matakwa ya Mwajiri na anakubali kwa hiari yake mwenyewe kuajiriwa kwa muda mfupi kama **KUCHIMBA MITARO KUJEGA VITUO VYA KUCHOTEA MAJI, KUJENGA CHEMBA ZA MAJI, KULAZA MABOMBA NA KUFUKIA KWA AJIRI YA KUSAMBAZA MTANDAO WA MAJI MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASWA.**

MKATABA HUU UNASHUHUDIA kwa pande zote mbili na kukubaliana kama ifuatavyo:

NYARAKA MUHIMU KATIKA MKATABA

1. Fomu ya Makubaliano
2. Barua ya Kukubariwa
3. Fomu ya Kuwasilisha Maombi ya Kazi
4. Nukuu za Bei
5. Mashariti ya Jumla
6. Utatuzi wa Migogoro

FOMU YA KUWASILISHA MAOMBI YA KAZI

Tarehe 10/11/2021

Kwa, MKURUGENZI MTENDAJI

MAMLAKA YA MAJI MASWA

> Nakubaliana kufanya kazi ya Kuchimba Miteno, Kulaza

bomba, kufukia, kujenga Chemba na ujenzi wa VITO

Yenye Nukuu Namba MAUWASA/2020/21/W/12

Kwa kiasi cha fedha ya Kitanzania MILIONI TITANANI NANNI LAHISTA

HAMSINI NAMBI (Kwa Maneno) NAMIATANU 84,652,500 (Kwa Tarakimu)

> Pia nakubali kufanya kazi hii kwa Kipindi cha MITATU (3) Siku/Miezi

> Nukuu hii ya bei na barua utakayoniandikia ya kukubaliwa, itakuwa inatengeza Mkataba Kati yangu na wewe.

> Pia nafahamu kwamba haulazimishwi kuchagua Fundi mwenye bei ya chini.

> Ninathibitisha kuwa Nukuu hii inakidhi masharti yanayotakiwa yakutangaza nukuu ya bei.

Saini B. Mwai popo

Jina BAHATI MWAIPOPO

Kazi FUNDI

Anuani S.P. 2968 MWANZA



Mchanganuo Wa Kazi Zinazotakiwa Kufanyika (BOQ)

Na:	Maelezo	Kipimo	Kiasi	Gharama	Jumla
1	Ujenzi wa chemba zenye saizi M1 x M1 kwa matofali ya saizi ya SM45 Xsm23 (Construction of chambers with size 1mx1mx1 by using blocks 45cm x 23cm as per engineering drawing)	Na.	10	70,000	700,000
2	Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji kama ilivyo kwenye michoro (Construction of DPS as per engineering drawing)	Na.	4	150,000	600,000
3	Kuuchimba mtaro wenye kina cha mita 1 na upana wa mita 0.5. kulaza bomba na kufukia za saizi zifuatazo :- <ul style="list-style-type: none"> • 25mm-150m • 63mm-13,000 • 110mm-2,500 • 160mm-6,000 	M	21,650	3850	83,352,500
Jumla					84,652,500



1. MADHUMUNI YA MKATABA

Mkataba huu ni kwa ajili ya **FUNDI MJENZI WA KUCHIMBA MITARO KUJEGA VITUO VYA KUCHOTEA MAJI, KUJENGA CHEMBA ZA MAJI, KULAZA MABOMBA NA KUFUKIA KWA AJIRI YA KUSAMBAZA MTANDAO WA MAJI MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASWA**

Ambapo Mwajiriwa atapaswa kufanya kazi zifuatazo:

1. Kuchimba Mitaro
2. Kujega Vituo Vya Kuchotea Maji.
3. Kujenga Chemba Za Maji.
4. Kulaza Mabomba ,Kuunganisha Na Kufukia

NB:Ujenzi na Uchimbaji huo utazingatia michoro na maelekezo kutoka kwa mwajiri.

2. MUDA WA UTEKELEZAJI WA KAZI

Kazi hij itafanyika kwa muda wa miezi ^{30/11/2021} 3. ambapo itaanza tarehe na itakamilika tarehe ^{28/02/2022} mwaka ²⁰²²

Kushindwa kukabidhi kazi hiyo ndani ya muda tajwa Mwajiri ana uwezo wa kuvunja mkataba ndani ya siku **saba(7)** baada ya tarehe ya mkataba kumalizika'

3. ONGEZEKO LA MUDA WA UTEKELEZAJI KAZI

- i. Kwamba mwajiriwa ana haki ya kuwasilisha ombi la muda wa nyongeza kwa mwajiri wake akitaja sababu zinazopelekea muda kuongezeka
- ii. Mwajiri atatafakari kwa kina ombi la mwajiriwa(fundi) na kutoa maamuzi yake bila kuingiliwa akitaja sababu za kuongeza au kutokuongeza muda wa utekelezaji endapo kama sababu ni sahihi au sio sahihi bila kuathiri gharama na muda wa mkataba
- iii. Mwajiriwa(fundi) anayo haki ya kuomba ongezeko la muda wenye tija na vifaa kwa ajili ya kutekeleza mabadiliko ya kimkataba kama upo ushahidi wa ongezeko ili kazi yote pamoja na mabadiliko ikamilike kwa ufanisi kwa taratibu za kiufundi.

4. MUDA WA MATAZAMIO

Mwajiriwa(fundi) atahakikisha anafanya marekebisho ya hitilafu zozote na kufanya mradi salama kipindi chote cha matazamio yasiku..... tangu tarehe ya kukamilisha kazi ndipo apewe hati ya ukamilishaji wa kazi na kuacha eneo la kazi safi na salama.

5. MABADILIKO MADOGO YA KAZI, KUONGEZEKA NA KUPUNGUA KWA KAZI

- i. Mwajiri kupitia kwa msimamizi wa kazi (Meneja mradi) ambaye ni mhandisi wa maji wa Mamlaka ya Maji anayo haki ya kufanya mabadiliko

ya aina yoyote pamoja na kuongeza au kupunguza kazi ndani ya asilimia kumi na tano **(15%) kwa kibali cha barua toka kwa mwajiri mwenyewe ,taratibu zote mabadiliko na si vinginevyo.**

- II. Mwajiriwa(fundi) atalazimika kuweka bei ya kazi ndogo amabazo zimeongezeka na ambazo viwango vyake(rates) hazipo katika makadirio ya kazi ya awali(BOQ) lakini kwa kazi ambazo zinapungua au kuongezeka na zipo ndani ya makadirio ya awali ya mkataba,bei halisi itapatikana kwa kutumia viwango vilivyo katika makadirio hayo ya kazi(BOQ) na si vinginevyo hata hivyo mabadiriko yoyote hayatakubaliwa bila mapatano ya kimaandishi kati ya pande zote mbili.

6. MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI

- 6.1 Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha **Tshs 81,405,000.00** Kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu;
- 6.2 Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni kwa fedha za kitanzania tu (*Tanzanian Shillings*);
- 6.3 Malipo hayo yatalipwa aidha kwa hundi ambayo italipwa benki;
- 6.4 Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kwa kuzingatia ubora na kiasi cha kazi zilizofanyika na kukamilika kwa mujibu wa BOQ iliyojazwa, yakiambatana na taarifa ya utekelezaji wa kazi (measurement of works) iliyosainiwa pande zote mbili.
- 6.5 Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa mara baada ya kukamilisha kazi ya ujenzi kama ilivyoainishwa katika kifungu **1** kifungu kidogo **(a)** kwa utaratibu ufuatao:
 - i. Malipo ya awali yatalipwa asilimia 10%
 - ii. Malipo awamu ya kwanza yatalipwa asilimia **20%** baada ya ukamilifu wa kazi usiopungua asilimia **20%** .
 - iii. Awamu ya pili (2) yatalipwa asilimia **30%** baada ya ukamilifu wa kazi usiopungua asilimia **65%** .
 - iv. Awamu ya tatu (3) Asilimia **30%** baada ya ukamilifu wa kazi usiopungua asilimia **95%**.
 - v. Awamu ya nne (4) Asilimia **10%** baada ya ukamilifu wa kazi kwa asilimia **100%**.
- 6.6 Kwamba malipo yanaweza kufanyika mara moja kama fundi mjenzi ana uwezo wa kutosha kutekeleza kazi hiyo pasipo kuomba malipo yoyote katika mchaganuo tajwa hapo juu anaweza kufanya kazi yote kwa ukamilifu na ubora kisha kuomba malipo yote kwa mara moja baada ya kazi kukamilika,kukaguliwa na kukubalika na mwajiri.

- 6.7 Kabla ya malipo ya mwisho kufanyika, Mwajiriwa anapaswa kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika na kufanya marejesho ya vifaa vyote vya kazi na fedha za mradi kama zitakuwepo.

7. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri ambaye atawakilishwa na Msimamizi wa Kazi, atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

- 7.1 Kutoa baadhi ya vifaa kwa ajili ya ujenzi wa kazi hii;
- 7.2 Kusimamia na kuthibitisha ubora wa kazi inayofanywa na fundi;
- 7.3 Kuwasiliana na uongozi wa eneo husika namna ya kuwashirikisha wananchi/Jumuiya ya Watumia Maji katika shughuli za ujenzi wa Mradi;
- 7.4 Endapo kazi itakayofanywa na Mwajiriwa haitafikia viwango vya ubora unaotakiwa, Mwajiri atachukuwa hatua stahiki dhidi ya Mwajiriwa huyo; na Msimamizi wa Mradi ata mtaarifu fundi wa kazi hii kwamba ameshindwa kutimiza masharti ya makubaliano.
- 7.5 Kuhakikisha kuwa endapo Mwajiriwa atafanya kazi isiyokidhi viwango au isiyoridhisha, Mwajiriwa huyo anarekebisha au kurudiwa upya kazi hiyo kwa gharama zake mwenyewe.

8. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRIWA

Mwajiriwa ambaye ni fundi atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

- 8.1 Kuhakikisha kuwa anatekeleza ujenzi wa kazi zote kama zilivyoelekezwa kwenye sehemu ya 1 (Madhumuni ya Mkataba) kulingana na ramani na vipimo vilivyotolewa na Mwajiri;
- 8.2 Kuhakikisha kuwa anawajibika kufanya kila jambo ambalo kwa ujumla wake litaleta mafanikio kwenye mradi atakaoujenga;
- 8.3 Atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, uadilifu, umakini na weledi mkubwa na endapo atatekeleza kinyume na matakwa haya, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake;
- 8.4 Atawajibika kwa Msimamizi wa Mradi (**Project Manager**) kwa utendaji wake wa kila siku na atatekeleza maelekezo anayopewa na kiongozi huyo;
- 8.5 Atawajibika kuhudhuria mikutano ya tathmini ya mradi pamoja na watendaji wengine wa timu yake kila itakapopangwa;
- 8.6 Atawajibika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi kabla ya malipo na kila zitakapohitajika;
- 8.7 Kuhakikisha malipo ya vibarua na mafundi walioajiriwa kwa mikataba midogo yanafanyika kwa wakati; na
- 8.8 Kufanya usafi eneo la ujenzi wa mradi na kuondoa mabaki yote ya vifaa vya ujenzi na kuviweka katika eneo litakaloelekezwa na Msimamizi wa Mradi.

9. UTOAJI WA MIKATABA MIDOGO

Mwajiriwa anaweza kuingia Mikataba midogo kiasi kadhaa ya utekelezaji wa kazi na vibarua (*casual labourers*) watakaokuwa chini ya usimamizi wake.

10. UCHELEWESHAJI WA UTEKELEZAJI WA MRADI

Endapo kazi haitakamilika katika muda uliopangwa, Mwajiriwa atalipa faini ya asilimia(0.01%) ya malipo ya kazi yote kwa kila siku ya ucheleweshwaji isipokuwa kukiwa na sababu ya msingi ya ucheleweshwaji wa kazi ulioidhinishwa kwa maandishi na Msimamizi wa Mradi.

11. DHAMANA YA UHARIBIFU

- 11.1 Mwajiriwa atawajibika kulipa gharama za uharibifu au madhara yoyote yatakayosababishwa na wafanyakazi wake au vifaa vyake wakati wa utekelezaji wa mradi; na
- 11.2 Gharama hizo au madhara hayo yatabainishwa na Msimamizi wa Mradi kwa maandishi.

12. SHERIA ITAKAYOTUMIKA

Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na Sheria za Tanzania.

13. USULUHISHI WA MGOGORO

Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote baina ya Mwajiri na Mwajiriwa kuhusu utekelezaji wa mradi huu:

- a) Pande zote mbili zitatatua mgogoro huo kwa njia ya amani ya mazungumzo ambapo makubaliano ya pande hizi mbili yatapelekea Mkataba huu kufanyiwa marekebisho; na
- b) Endapo mgogoro huo utashindikana kutatatuliwa kwa njia ya amani ya mazungumzo, pande zote mbili zinaweza kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

14. KUSITISHA MKATABA

Mkataba huu unaweza kusitishwa endapo upande mmoja au pande zote mbili za Mkataba zitashindwa kutekeleza wajibu wake au masharti ya Mkataba huu.

15. MAREKEBISHO YA MKATABA HUU


Kwamba Mwajiri na Mwajiriwa wanaweza kubadilisha baadhi ya masharti ya Mkataba huu kwa makubaliano ya pamoja kwa njia ya maandishi.


KWA USHUHUDA HUU, pande zote mbili zinaweka sahihi zao katika Mkataba huu siku na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:

KWANIABA YA MWAJIRI (MASWA-WSSA) Shahidi:

Jina: NANSI MATIAS

Jina: JERMS UMATI

Sahihi: 


Sahihi: 

Cheo: Mkurugenzi Mtendaji

Cheo: APESA UJAWI

Tarehe: 17/11/2021

Tarehe: 17/11/2021




KWANIABA YA MWAJIRIWA (FUNDI)

Shahidi:

Jina: BAHATI LUCAS MWAIPPO

Jina: NEMEL PETER

Sahihi: 

Sahihi: 

Cheo: FUNDI

Cheo: fundi

Tarehe: 17/11/2021

Tarehe: 17/11/2021



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF WATER
MASWA WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY

Telegrams "MAJI Tel No: 028-2750237/2750375
S.L.P 185, Maswa
Fax: 028-27502337, email: mdmauwa@a@maji.go.tz



NEGOTIATION MEETING

Project: CONSTRUCTION OF EXTENSION LINE FOR MASWA-WSSA

MINUTES OF THE MEETING 16/11/2021

1. Detail of the meetings

Venue MANAGING DIRECTOR OFFICE

Date: 16/11/2021

Time 12:20- 01:31


2. Participants

Name	Organization	Position	Department	Signature
Jonas kimath	MASWA-WSSA	Procurement and supplies officer	0765764574	
Leonard Mnyeti	MASWA-WSSA	Technical Manager	0757732911	
Raphael Mwita	MASWA-WSSA	Production Manager	0768219951	
Boniface Kasinde	MASWA-WSSA	Commercial Manager	0754710930	
Patrick Urio	MASWA-WSSA	Network Incharge	0754480112	
Bahati Lucas Mwaipopo	Local fundi	Local fundi	0765003002	

S/N	MEETING AGENDA	Resolution
	1: Opening Of the Meeting 2: Brief Description Of The Project 3: Negotiation Discussion 4: AOB 5: Closing the meeting	
1.0	<p>Opening Of the Meeting</p> <p>The Chairman opened the meeting at 12.20 hours by welcoming the Members of the negotiation team and the local fundi, and gave them opportunity to introduce themselves. After such a brief self-introduction, he introduced the main agenda of this meeting is to discuss and clarify some issues which were not apparent or could not be finalized at the time of bidding.</p>	
2.0	<p>Brief Description Of The Project:</p> <p>The briefing of the project was presented by head of Technical Department , who explain brief the scope of work is to Trench excavation with maximum depth of 1m and 0.45 m width, Lay HDPE pipe with different size by joining by batty fusion test 21,650 meters, backfill and compact well with selected soil , Construction of chambers with size 1mx1mx1 by using blocks 45cm x 23cm as per engineering drawing) and Construction of DP'S as per engineering drawing</p>	<p>Recommended</p>
3.0	<p>Contract price :</p> <p>After deeply discussion between the Local Fundi and negotiation committee, the Local Fundi agreed to lower the price from Tshs 84,652,500 to Tshs 81,405,000.</p>	<p>Recommended</p>

4.0	<p>Inspection and testing materials:</p> <p>Inspection and testing of material shall be conducted by the team appointed by Managing Director.</p>	Recommended
5.0	<p>Time frame for completion of work :</p> <p>The time agreed by both parties for completion of the project shall not exceed three months.</p>	Recommended
6.0	<p>Payment modality :</p> <p>I was agreed that the payment certificate will as follows;-</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Advance payment 10 total amount of the work 2. Second phase payment will be 20% after construction work 20% 3. Third phase payment will be 30% after construction work 65% 4. Fourth phase payment will be 30% after construction work 95% 5. Fifth phase payment will be 10% after construction work 100% 	Recommended


7.0	Advance payment : The client agreed to pay 10% Advance Payment.	Recommended
8.0	AOB The chairperson insisted the Local Fundi to maintain the quality of work and to abide with specification and engineering drawing Issued by MASWA-WSSA contraction committee also to maintain Time schedule	Recommended
9.0	Closing: The Chairman expressed his gratitude to all the Members for attending the meeting and their cooperation during the negotiation process. He finally closed the meeting at 01.31 hours.	Recommended



Secretary

16/11/2024

Date



Chairman

16/11/2024

Date